

Mbinu za Ujenzi wa Wahusika na Usawiri wa Sifa Zao: Uhakiki wa Riwaya ya *Dunia Uwanja Wa Fujo* ya E. Kezilahabi

Leonard Flavian Ilomo

Ikisiri

*Kipengele cha wahusika ni muhimu katika kuunda kazi yoyote ya kifasihi. Kipengele hiki hushirikiana na vipengele vingine vya kifani katika kutoa maudhui ya kazi yoyote ya kifasihi. Kwa kawaida wahusika hujengwa kisanaa na mwandishi ili waweze kuwakilisha dhana mbalimbali za maisha katika jamii (Msokile 1992). Mwandishi huwajenga wahusika wake kwa kutumia mbinu mbalimbali ili kuwatofautisha na hivyo kuiwezesha hadhira yake kutambua sifa au tabia za mhusika fulani zinazomtofautisha na mhusika mwininge katika kazi husika. Hata hivyo, ni vema ifahamike kuwa kila msanii wa kazi ya kifasihi ana mbinu zake za kuwajenga wahusika wake. Hii ina maana kuwa, msanii wa kazi ya kifasihi anaweza kutumia mbinu moja au zaidi katika kazi fulani kutegemeana na aina ya utanzu anaoushughulikia. Kwa kutambua hoja hiyo, makala haya yanafafanua mbinu mbalimbali zilizotumiwa na E. Kezilahabi katika kuwajenga wahusika katika riwaya ya *Dunia Uwanja wa Fujo* na mchango wa kila mbinu katika kubaini sifa za wahusika pamoja na dhamira katika kazi hiyo. Makala hii imegawanyika katika sehemu nne. Sehemu ya kwanza ni utangulizi unaotoa muhtasari kuhusu riwaya ya *Dunia Uwanja wa Fujo*; sehemu ya pili inazungumzia dhana ya wahusika katika fasihi; sehemu ya tatu inajadili mbinu mbalimbali zinazotumika kuwajenga wahusika na jinsi sifa za wahusika zinavyosawiriwa kupitia mbinu hizo; na sehemu ya nne ni hitimisho la mjadala katika makala hii.*

1.0 Utangulizi

Kuna tahakiki na maelezo mbalimbali kuhusu riwaya ya Kezilahabi, *Dunia Uwanja wa Fujo*. Tahakiki hizo zimefanywa na wahakiki mbalimbali wa fasihi huku kila mmoja akiwa na mwelekeo wake kutegemea lengo la mhakiki husika. Suala hili pia analigusia Mlacha (1991) kuwa, uchunguzi wa riwaya unaweza kufanywa kwa kuzingatia vipengele tofautitofauti kwa kutegemea kile ambacho mhakiki anakusudia kukichunguza. Miiongoni mwa wahakiki hao ni Senkoro (1982, 2011), Mulokozi (1983), Wamitila (1997), Wafula (2002) na Diegner (2002).

Senkoro (1982, 2011) na Mulokozi (1983), wanaihakiki riwaya ya *Dunia Uwanja wa Fujo* kwa kujikita zaidi katika maudhui yake. Senkoro (keshatajwa) anafafanua kuwa, riwaya hii inashughulikia migogoro, matatizo na mikinzano ya kijamii, kiuchumi na kifalsafa katika jamii ya Tanzania baada ya kutangazwa kwa Azimio la Arusha. Mulokozi (keshatajwa) anaenda mbali kidogo kwa kufafanua viwango ambavyo tatizo la maisha katika riwaya hii linavyojadiliwa. Anavifafanua viwango hivyo kuwa ni kiwango cha mtu binafsi na kiwango cha jamii. Wamitila (1997) katika makala yake “*Contemptus Mundi and Carpe Diem Motifs in Kezilahabi’s Works*” anaielezea riwaya ya *Dunia Uwanja wa Fujo* kuwa ni mfano bora wa motifu ya dunia kama mahali pabaya pa kuishi na kuwa kuanzia mwanzo mwandishi anachora picha ya ulimwengu ulio duni na usioaminika: sehemu yenye fujo ambapo utu unafifia katika

mateso. Ubaya wa ulimwengu kama inavyooneshwa katika riwaya hii unatokana na uzinzi, unyonyaji, ukahaba, kushushwa thamani kwa asasi ya ndoa, maamuzi yasiyozingatia maoni ya wengine, dharau na visasi.

Kwa jumla tunapochunguza tahakiki hizo kuhusu riwaya ya *Dunia Uwanja wa Fujo*, tunagundua kuwa zimejikita zaidi katika kuchunguza maudhui. Suala hili linajitokeza si katika riwaya hii tu, bali linajitokeza pia katika tahakiki nyingi, hususan katika taaluma ya fasihi ya Kiswahili (Mohochi, 2000). Hivyo, katika makala haya tunachunguza kipengele cha fani cha riwaya ya *Dunia Uwanja wa Fujo*, hususan wahusika kwa kuangalia mbinu zilizotumika kuwasawiri na jinsi mbinu hizo zinavyosaidia kuyaelewa maudhui.

2.0 Dhana ya Wahusika

Wahusika wana umuhimu mkubwa katika kuiunda simulizi ya kifasihi. Hii inatokana na ukweli kuwa, wahusika huweza kuathiri simulizi inayosimuliwa, yaani wao ndio hupeleka mbele matukio katika simulizi. Wahusika wanaelezwa kuwa ni sehemu muhimu ya fani (Msokile, 1992; Njogu & Chimerah, 2008), na kwamba, wahusika ni viumbe wa kisanaa wanaobuniwa kutokana na mazingira na malengo ya msimulizi. Bal (1997) anaeleza kuwa, wahusika hushabihiana na watu kwa kuwa fasihi huandikwa kwa ajili ya watu na kwa hiyo huwahuwu watu hao. Kwa kawaida wahusika si watu halisi, bali ni matokeo ya ubunifu wa msanii ili kuakisi masuala kadhaa ya kijamii ambayo msanii ameyakusudia. Kuhusu hili Bal (khj: 115) anasema:

“They are fabricated creatures made up from fantasy, imitation, memory: paper people, without flesh and blood...The character is not a human being, but it resembles one. It has no real psyche, personality, ideology or competence to act but it does possess characteristics which make psychological and ideological description possible”.

Wahusika ni viumbe wa kubuni wanaotokana na fantasia, mwigo, na kumbukumbu: ni watu bandia wasio na damu na nyama...Mhusika si binadamu lakini anafanana na binadamu. Hana akili, haiba, itikadi wala uwezo wa kutenda bali ana sifa zinazotuwezesha kumtolea maelezo ya kisaikolojia na kiitikadi (Tafsiri Yetu).

Katika maelezo hayo, kinachojidhihirisha ni kukosekana akili, haiba, itikadi, na uwezo wa kutenda kwa wahusika hali inayowafanya kuwa viumbe wa kubuni; yaani, wanaotokana na ubunifu wa msanii ambaye huwaumba kufuatana na malengo yake. Maelezo haya yanaungwa mkono na Mohamed (1995:72) anayesema, “*mwandishi anapoumba wahusika wake anaumba watu wasioishi katika ulimwengu wetu wa bayana, bali wenyewe kuishi katika ulimwengu wao wa hadithi au tamthilia ambamo wakitolewa watakuwa hawana maisha...*”

Madumulla (2009) akiwarejelea Kasper na Wuckel (1982) anaeleza kuwa, mhusika ni picha ambayo huchorwa na fasihi na ni kiini cha vitu vyote vipyta, dhamira na mada katika fasihi. Anaendelea kueleza kuwa, katika mhusika kuna uwili: mosi, kuna usawiri wa kisanaa wa mtu kwa upande mmoja; pili kuna sura ya mtu kwa upande mwininge. Ufafanuzi huu unashadidia hoja tuliyooita hapo awali kuwa, wahusika si watu halisi bali watu wa kubuni. Ubunifu wa msanii humuwezesha msanii kuwaumba au kuwasawiri wahusika kinafsia, kiakili, na kimwili. Usawiri wa wahusika unaofanywa na msanii hutegemea mbinu mbalimbali ambazo msanii huyo amezitumia. Kwa kuzingatia kauli hiyo, katika kipengele kinachofuata tumbainisha mbinu mbalimbali ambazo msimulizi-mwandishi amezitumia katika kuwajenga wahusika wa simulizi yake ya *Dunia Uwanja wa Fujo*. Mbinu hizo ni matendo, mazingira, matamshi, uzungumzinafsiya, mazungumzo baina ya wahusika, na uwasilishaji dhahiri.

3.0 Mbinu za Ujenzi wa Wahusika

3.1 Mbinu ya Kimatendo

Hii ni mionganoni mwa mbinu ambazo msimulizi-mwandishi amezitumia katika kuwajenga wahusika wa simulizi yake. Kwa kawaida matendo ya mhusika yanaweza kuainishwa katika makundi matatu kama asemavyo Rimmon-Kennan (2002) ambaye ananukuliwa na Shen (2006). Makundi hayo ni: tendo linalotendwa na mhusika “*act of commission*,” tendo ambalo mhusika anapaswa kulitenda lakini halitendi “*act of omission*,” na tendo ambalo halijafanikiwa ingawa mhusika amekusudia kulifanya “*contemplated act*.” Mbinu hii humfanya msimulizi atumie ufanuzi kidogo huku msimuliwaji akipewa nafasi kubwa ya kutafsiri maana na sifa au tabia ya mhusika kutokana na matendo yake. Msokile (1992:43) anaeleza kuwa, “*msanii huwaunda* wahusika kwa kutoa matendo nusunusu, hatoi maelezo juu ya matendo yote kwa mara moja.” Katika riwaya ya *Dunia Uwanja wa Fujo*, mbinu ya matendo imetumika katika kuwajenga wahusika.

Tumaini ni mionganoni mwa wahusika ambao wamejengwa kwa kutumia mbinu hii ya matendo. Katika riwaya hii tunasimuliwa kuwa Tumaini alimtorosha Anastasia, binti wa Mulele na mkewe Bukehele ili asiweze kuozwa kwa Tembo, mtu aliye kuwa mume wa marehemu dada yake Anastasia. Tunasimuliwa kuwa, Tumaini alifanikiwa kumtorosha na kwenda kuishi naye Shinyanga bila idhini ya wazazi wake Anastasia. Kutokana na kitendo hiki tunaweza kumuelezea Tumaini kama mtu aliye kuwa hajali taratibu za jamii yake na pia kitendo hiki kinadokeza mgogoro kati ya vijana na wazee, mgogoro ambao ni matokeo ya vijana kujitafutia uhuru wao katika masuala mbalimbali. Kitendo hiki cha Tumaini kumtorosha Anastasia kinaingia katika tendo linalotendwa na mhusika kama inavyoelezwa na Shen (keshatajwa) ambaye

anamnkuu Rimmon-Kenan. Kitendo hiki cha Tumaini kinajidhihirisha katika ukurasa wa 48 wa riwaya hiyo kama ifuatavyo:

Anastasia alikuta Tumaini anafika kutoka mjini kupeleka vitu vyake. Tumaini alimbeba Anastasia kwa baiskeli kuelekea Lutare. Njiani Tumaini alimweleza Anastasia mpango aliokuwa nao. Anastasia alisikiliza kwa makini.

“Anastasia, unafahamu nimekuleta huku ngomani kwa sababu wazazi wako hawataweza kuvumbua ni nani amekutorosha...”

Zaidi ya kitendo chake cha kumtorosha Anastasia, Tumaini alifanya kitendo cha mauaji baada ya kumpiga kwa risasi mkuu wa wilaya aliyejewa akihutubia mukutano kuhusu ujamaa amba Tumaini aliupinga. Tumaini alimpiga kwa risasi mkuu wa wilaya baada ya mashamba yake kutaifishwa na kugeuzwa kuwa mali ya kijiji cha ujamaa. Hiki ni kitendo ambacho kinamsawiri Tumaini kama muuaji na hivyo kuibua dhamira ya mauaji. Hili linajitokeza ukurasa wa 128 ambapo tunasimuliwa:

Kelele za watu zilikuwa hazijatulia mlion wa bunduki uliposikika. Hapo hapo Mkuu wa Wilaya alitotoma chini akaanguka. Mlio wa pili ulisikika pale pale. Tumaini ambaye alikuwa akijaribu kutoroka alianguka chini. Watu wakasambaa ovyo huko na huko kwa mbio. Kila mtu akajua roho yake. Uwanja wa mpira ukawa mdogo; mlanga ukawa hauonekani, na ukuta ukawa mfupi.

Katika dondo hilo tunaona Tumaini akijaribu kutoroka baada ya kumpiga Mkuu wa Wilaya kwa risasi, kitendo ambacho kinamfanya akamatwe na baadaye kuhukumiwa kunyongwa. Pia, kitendo cha Tumaini kutozingatia ushauri wa mama yake, ushauri uliomtaka kutafuta mchumba kwa kuzingatia tabia njema na kisha kuoa kinamsawiri Tumaini kama mtu mkaidi, na pia kinaibua dhamira ya kiburi na umalaya. Katika riwaya hii tunasimuliwa kuwa, badala ya kutafuta mchumba na kuoa, Tumaini alijishughulisha zaidi na kutembea na wasichana tofauti tofauti pale kijijini kama inavyosimuliwa katika ukurasa wa 17 kuwa:

Wasichana wengi kijijini walimpenda. Siyo kwa sababu alikuwa na pesa lakini kwa sababu walimwona ni mwenzao: Tumaini hakuwa na kazi ya ofisini. Kwa hiyo aliweza kuwaoa. Kule tu kutaja jina lake kulimfanya kila msichana kijijini awe na tumaini la kuolewa naye.

Mama Resi ni mhusika mwengine ambaye amesawiriwa na msimulizi-mwandishi kwa kutumia mbinu hii ya matendo. Kitendo kimojawapo ambacho alikifanya mhusika huyu ni kile cha kukataa kushuka kwenye basi, ‘*Tanganyika Bus*,’ ili abiria wengine wasukume basi hilo lililokwuwa limekwama matopeni. Kitendo hiki cha kukataa kushuka kwenye basi kinamsawiri mhusika huyu kama mtu mwenye kiburi na dhara. Katika ukurasa wa 57 msimulizi-mwandishi anatusimulia:

Zilikuwa zimebaki maili arubaini kufika Shinyanga basi lilipokwama matopeni. Watu wote waliombwa kutoka nje abaki dereva ndani peke yake. Watu wote walitoka nje lakini yule mama na mtoto wake alikataa kutoka nje.

Kitendo hiki cha Mama Resi kinasawiri sifa ya kiburi aliyokuwa nayo mhusika huyo na pia kinaibua dhamira ya ukaidi. Aidha, katika ukurasa wa 70 tunaona msimulizi-mwandishi anaendelea kutumia mbinu ya kimatendo kumsawiri Mama Resi. Katika ukurasa huo tunaelezwa matendo ya Mama Resi ya kuwa anaosha vyombo nusu saa kabla ya kula. Tunasimuliwa kuwa:

Ukifika nyumbani kwa Dennis hukosi kukuta vyombo vimewekwa nje bila kuoshwa. Kwa Dennis vyombo huoshwa nusu saa kabla ya kula hata vyombo vilivytumika usiku.

Kitendo hicho cha kuacha kuosha vyombo kwa muda mrefu, zaidi ya kumsawiri Mama Resi kama mtu mvivu na mzembe, pia kinasaidia kuibua dhamira ya uvivu na uzembe mionganoni mwa wanajamii. Aidha, kupitia mpango ambao Mama Resi alishiriki kuuandaa, mpango wa kumuua Tumaini kwa sababu tu ya kutopenda maendeleo yake, unamsawiri Mama Resi kuwa mtu mwenye wivu, roho mbaya na mwuaji. Pia, kitendo hicho cha Mama Resi kinaibua dhamira ya wivu na mauaji. Hata hivyo, tunasimuliwa kuwa mpango wa kumuua Tumaini ulishindikana baada ya washiriki wa mpango huo kutolewana. Kitendo hiki kinaingia katika ile aina ya tendo ambalo mhusika anakusudia kulitekeleza lakini linashindikana kutekelezwa.

“Tukishatenda jambo lazima tulitimize. Hatuwezi kuacha mambo nusu nusu. Angalieni sasa tumo matatizoni. Huenda tukanyongwa au kufungwa maisha!” Mama Resi alisema maneno hayo kwa kelele. Alitoa shilingi mia tano na kuzitupa chini. “Bwana Makoroboi! Chukua hizo pesa. Mimi nataka uniletee kichwa chake!” (ukurasa wa 88).

Katika maelezo ya dondo hilo tunaona Mama Resi akinung’unika baada ya mpango wao wa kumuua Tumaini kushindikana.

3.2 Mbinu ya Matamshi

Katika mbinu hii msimulizi huwajenga wahusika kwa kuwafanya wazungumze ili lafudhi zao ziweze kuwabainisha. Kwa mfano, katika simulizi fulani msimulizi-mwandishi anaweza kumjenga mhusika wake kwa kumfanya azungumze kwa lafudhi ambayo ni tofauti na wahusika wengine ili kumtofautisha na wahusika wengine. Lafudhi itakayosikika kutoka kwa mhusika huyo huweza kusawiri usuli wake na kuibua dhamira fulani.

Katika riwaya ya *Dunia Uwanja wa Fujo* mbinu hii imetumika katika kumjenga Kasala ambaye anaonekana kuongea Kiswahili ambacho kimeathiriwa na lugha yake ya asili. Katika ukurasa wa 5 msimulizi-mwandishi anatusimulia:

Polisi walipokuja walimkuta ameinama kichwa, damu ikimtoka puan.

“Mzee! Umekuwaje!” walimwuliza.

“Batoto bamenisondogorasondogora na chichwa! Bengine bamenikorotorakorotora na kucha!” alijibu kwa Kiswahili alichokuwa anazungumza siku zile.

“Walikupiga kwa hedi labda?”

“Hapana na chichwa!”

“Na ngumi na makofi!”

“Ndiyo balikuwa kumi na kofia!”

Katika mazungumzo hayo inabainika wazi kuwa matamshi ya Kasala, yaani jinsi alivyokuwa akitamka maneno yake, na wale polisi yalikuwa tofauti. Kwa mfano, dondoo hilo linaonesha neno ‘kichwa’ lilitamkwa kama ‘chichwa’, ‘walikuwa’ lilitamkwa kama ‘balikuwa’ na kadhalika. Zaidi ya matamshi inaonekana Kasala alishindwa kuelewa maana ya neno ‘ngumi’ kwa kudhani ni ‘kumi’, na ‘makofi’ kwa kudhani ni ‘kofia’. Kwa hiyo, kutokana na matamshi yake Kasala anasawiriwa kama mtu aliyejewa hajui lugha ya Kiswahili vizuri. Zaidi ya kumsawiri kama mtu aliyejewa hajui Kiswahili vizuri, mbinu hii ya matamshi inasaidia kubainisha tofauti za watu kijiografia na kuibua dhamira ya tofauti baina ya miji na vijiji. Matamshi ya Kasala yanaibua dhamira hii kutokana na ukweli kuwa katika jamii za Kitanzania, watu waishio vijijini matamshi yao ya lugha ya Kiswahili huwa yameathiriwa sana na lugha za makabila tofauti na watu waishio katika miji ambako lugha za makabila hazipewi nafasi kubwa katika mawasiliano ya kila siku.

3.3 Mbinu ya Kimazingira

Mbinu hii inajitokeza zaidi tunapozichunguza tabia mbalimbali za Tumaini ambazo ni matokeo ya mazingira aliyoishi hapo awali. Katika ukurasa wa 11 tunasimuliwa:

Tumaini alikuwa kwa kutengwa. Alinunuliwa vijigari vidogo vingi; kila alicholilia alipewa. Siku moja Tumaini alimchoma mlezi wake jichoni. Yule mvulana alimpiga Tumaini kidogo. Tumaini alikimbia kwenda kushitaki kwa mama yake.

Kutokana na maelezo hayo tunapata picha nzima ya mazingira ambayo Tumaini alilelewa. Tunaelezwa kuwa Tumaini alikulia katika mazingira ya kuengwa sana, yaliyomfanya awe na tabia zisizokubalika. Ni kutokana na malezi hayo, Tumaini alijenga dharau kwa watu wengine. Pia, tunasimuliwa kuwa, zaidi ya mazingira ya kuengwa Tumaini alikulia katika mazingira ya uyatima baada ya wazazi wake kufariki na ndugu zake kutokuwa tayari kuishi naye. Katika ukurasa wa 16 tunasimuliwa:

Baada ya kifo cha mama yake, Tumaini alikata shauri kuacha shule...Tumaini alipoacha kusoma alishi ndani ya nyumba ya baba yake. Marehemu baba yake

alikuwa hakai ndani ya nyumba za serikali...Tumaini alirithi shilingi elfu hamsini. Kwa sababu hii jamaa zake walikataa kuja kuishi naye.

Maelezo hayo yanaendelea kufafanua mazingira aliyokulia Tumaini, mazingira ya uyatima ambayo yalimsababisha akose mwongozo katika maisha yake. Hali hii ilimfanya Tumaini aishi kwa kujiongoza mwenyewe. Pamoja na mazingira magumu aliyoishi, tunaelezwa kuwa Tumaini alipambana na mazingira hayo na hatimaye alifanikiwa ingawa Azimio la Arusha lilimpotezea matumaini yake. Kwa hiyo, kutokana na mazingira hayo matendo ya baadaye ya Tumaini yaliathiriwa sana. Kwa mfano, mazingira ya kuengwa yalisababisha Tumaini aamini kuwa kila alichokifanya kilikuwa ni sahihi na kwamba ilikuwa ni haki yake. Hali hii ilimfanya Tumaini kuwa kiumbe aliyetenda kinyume na matarajio ya jamii iliyomzunguka kwa sababu ya kiburi na dharau. Mbinu hii ya kimazingira, zaidi ya kumsawiri Tumaini kama yatima pia inaibua dhamira ya malezi na umuhimu wa wazazi.

3.4 Mbinu ya Uzungumzinafsya

Wamitila (2008:379) anaifafanua mbinu hii kuwa ni “mtindo wa kuyawasilisha mawazo ya mhusika kwa mtindo au njia ya kujizungumzia.” Anaendelea kueleza kuwa, “katika uchunguzi wa dhana hii tunaweza kubainisha kati ya aina kuu mbili: (a) uzungumzinafsya wa moja kwa moja, na (b) uzungumzinafsya usio wa moja kwa moja...” Kutokana na maelezo hayo tunaweza kueleza kuwa, uzungumzinafsya unahusu monolojia, yaani mhusika anajizungumzia peke yake. Kutokana na kujizungumzia huko, wasimuliwaji hupata fursa ya kufahamu kile kinachoendelea katika akili ya mhusika, kwa hivyo wasimuliwaji huweza kubaini sifa au tabia za mhusika huyo pamoja na maudhui yanayoibuliwa.

Katika riwaya ya *Dunia Uwanja wa Fujo* mbinu hii imetumiwa na msimulizi-mwandishi katika kuwajenga baadhi ya wahusika wake. Miongoni mwa wahusika wanaojengwa kwa mbinu hii ni Mugala. Huyu alikuwa mama yake Kasala ambaye alihamishiwa kisiwani kutokana na kuhisiwa kuwa alikuwa mchawi. Msimulizi-mwandishi anatumia mbinu hii katika kumsawiri Mugala katika ukurasa wa 19 anasema:

Tumaini alipofika mbali sana, Mugala alianza kucheka hali akizungumza polepole. Sasa ilikuwa zamu yake kumcheka mwensiwe.

“Samaki amejileta mwenyewe ndani ya chungu. Kenge akikosa chakula huachama; nzi wakiona mdomo wake mwekundu hufikiri ni nyama na kuingia kwa wingi. Akiona wamekuwa wengi hufunga mdomo na kuwatafuna. Nimekwishakata shauri kuumaliza ukoo wao. Na nitaumaliza. Lakini, huyu mtoto ni mzuri vile kwamba nimemwonea huruma. Oh! Ninakumbuka katika kazi yetu huruma ni kosa kubwa

sana. Siku ile niliyoapa msituni, kwa kuuma kidole gumba, kwamba sitamhurumia mtu yejote bado naikumbuka. Kwa hiyo nitamchukua mtoto huyu. Lakini hakuna haraka. Nitamwacha kwa muda afanye mapenzi yake na Leonila.”

Katika dondo hilo tunamwona Mugala akijizungumzia peke yake baada ya Tumaini kuondoka. Huu ni uzungumzinafsiya wa moja kwa moja kutokana na mawazo ya Mugala kuweza kubainika wazi bila kuingiliwa na mtunzi. Kutokana na kujizungumzia huku, tunabaini kuwa Mugala ni muuaji tena asiyé na huruma kunatokana na kiapo alichokula msituni. Zaidi ya kumsawiri Mugala, mbinu hiyo inaibua dhamira ya uchawi na ushirikina.

Tumaini ni mhusika mwingine ambaye amesawiriwa kwa kutumia mbinu hii ya uzungumzinafsiya. Katika ukurasa wa 19 tunasimuliwa kuwa, akiwa njiani kutoka katika mji wa Kasala kuonana na Mugala, Tumaini alisikia kama sauti ya ndege akiimba. Hata hivyo, sauti hiyo haikuwa ya ndege bali ilikuwa sauti ya moyo wa Tumaini. Katika ukurasa huo tunasimuliwa:

Akiwa njiani kurudi nyumbani, Tumaini alisikia sauti kama ya ndege akiimba kwa huzuni: “Tumaini usidhani kwamba umefanya jambo zuri. Huyo mzee amekwisha kuwa kama mtoto mdogo. Wewe umemchezea kama picha. Tumaini, hii ndio heshima yako kwa watu kama hawa! Tumaini huna huruma; utakuja kuwa kama yeje siku moja!”

Hiyo haikuwa sauti ya ndege. Sauti ya moyo wake ndio ilikuwa ikisumbua.

Tunapochunguza dondo hilo tunabaini kuwa, Tumaini alikuwa akijizungumzia nafsi mwake. Huu ni uzungumzinafsiya usio wa moja kwa moja kwa sababu sauti inayosikika ni ya msimulizi nafsi ya pili. Uzungumzinafsiya huu unatuwezesha kubaini sifa ya utovu wa nidhamu aliokuwa nao Tumaini na umuhimu wa kuheshimu wazee. Ni kutokana na kugundua kuwa alimkosea Mugala, alianza kujuta yeje mwenyewe.

Tumaini anaendelea kusawiriwa na mbinu hii katika ukurasa wa 32 ambapo anaonekana akitafakari kitendo cha wanakijiji kumnyanyasa Mugala na hatimaye kuhamishiwa katika kisiwa cha wachawi. Tukio hili linamfanya Tumaini atafakari mwenendo mzima wa maisha yake na hatima yake pale kijijini. Katika ukurasa huo tunasimuliwa:

Alipofika kitandani mawazo mengi yalimwingia kichwani. Alianza kufikiri.

“Nafikiri Mugala alikuwa mtu mwema, hasa kwangu. Alinisaidia kupata chakula nilipokuwa nina njaa. Lakini kwa muda wa siku moja tu amechukiwa na kila mtu kwa ajili ya matendo yake mabaya. Mtu ambaye ameshindwa kuishi na raia amechoka maisha. Huu ni ukweli mtupu. Mugala alipigwa na watoto wadogo,

alitemewa mate, lakini hata jamaa zake walimtazama tu. Kumbe raia wakikususa unakuwa kama mnyama! Mimi je? Huenda labda watu wamekwishaanza kunikasirikia kwa kuharibu binti zao! Kuna mambo mawili ninayoweza kufanya; au nirekebishe mwenendo wangu na niendelee kuishi humuhumu kijijini; au nitoroke niende nchi za mbali kabla mtumbwi haujatoboka..."

Katika dondoo hilo tunaona Tumaini akijizungumzia peke yake. Kujizungumzia huko kunatokana na matendo aliyofanyiwa Mugala, matendo ambayo yanamfanya Tumaini ajitathimini mwenendo wake na hatima yake pale kijijini. Kutokana na dondoo hilo Tumaini anasawiriwa kama mtu aliyejikuwa na uwezo wa kugundua hatari inayomyemelea na ambaye alikuwa akiujua ukweli lakini alikuwa akiupuuuzia. Pia, kutokana na kujizungumzia huko tunajuzwa umuhimu wa kuishi vizuri na watu. Zaidi ya dondoo hilo, katika ukurasa wa 120 msimulizi-mwandishi anaendelea kumsawiri Tumaini kwa kutumia mbinu hii. Katika ukurasa huo tunasimuliwa kuwa:

Alipokuwa akiosha vyombo, Tumaini alikuwa ameshindwa kupata usingizi. Alikuwa sasa akizungukazunguka humo chumbani. Mawazo haya yalikuwa yakimzunguka kichwani.

"Siwezi kutukanwa na mwanasiasa anayetegemea kura yangu! Haiwezekani! Mimi sikumkataza kunenepa! Na hata hivyo ninakula jasho langu. Tabu nilioipata zamani imenifunza kutafuta pesa. Nilikata shauri kufanya kazi; nikawa nashinda shambani asubuhi na jioni. Na sasa nimepata mali. Halafu huyu mwanasiasa ananiita mnyonyaji! Mali niliyosumbukia mwenyewe wakati watu wengine walikuwa wakishinda kwenye kangara! Haiwezekani! Potelea mbali vijiji vyao vya ujamaa ambavyo vimerudisha nyuma maendeleo ya watu wengi. Haiwezekani!"

Katika dondoo hii msimulizi-mwandishi anamchora Tumaini akijizungumzia. Katika kujizungumzia huko, Tumaini anatuwezesha kutambua msimamo wake kuhusu sera ya vijiji vya ujamaa ambavyo vilikuwa ni matokeo ya Azimio la Arusha. Hivyo, mbinu hii inamjenga au kumsawiri Tumaini kama mtu aliyejikuwa akipinga sera ya vijiji vya ujamaa kwa sababu aliamini kuwa vijiji hivyo vilikuwa vikirudisha nyuma maendeleo. Zaidi ya kumsawiri Tumaini, mbinu hii inaibua dhamira ya suala la upokezi wa Azimio la Arusha mionganoni mwa Watanzania. Katika dondoo hilo inaonekana kuwa Azimio la Arusha lilikumbana na upinzani wa wanajamii kama anavyofafanua Senkoro (2011:88), "kwa wakulima, kwa vile hawa ni tabaka lililo gumu sana katika kubadili wenendo wake na kaida zake za maisha; ilikuwa vigumu kwao kulipokea Azimio kwa urahisi."

3.5 Mbinu ya Mazungumzo baina ya Wahusika

Mbinu hii imetumika kwa kiasi kikubwa katika riwaya ya *Dunia Uwanja wa Fujo*, ambapo msimulizi-mwandishi amewapambanisha wahusika ili wazungumze wao kwa

wao. Msokile (keshatajwa:44) anaeleza, “kadiri wanavyoendelea, wazo la mhusika pamoja na tabia yake hujulikana taratibu katika kazi hiyo.” Katika riwaya hiyo, wahusika mbalimbali wamejengwa au wamesawiriwa kwa kutumia mbinu hii. Mionganini mwa wahusika hao ni Mama Resi na Tumaini. Katika riwaya hiyo, msimulizi-mwandishi amewapambanisha wahusika hawa katika sehemu mbalimbali za simulizi yake. Kwa mfano, katika ukurasa wa 71 Tumaini anaoneka akizungumza na Mama Resi kama ifuatavyo:

“Imekwendaje hata ukaoa msichana ambaye hakusoma?”

“Ni mapenzi tu, Mama Resi.”

“Mapenzi gani hayo! Mimi ninafahamu kwa nini umemwoa. Umemwoa ili uweze kumwonea. Unataka mwanamke ambaye unawenza kumwamrisha kama mtoto mdogo, karibu kama mtumwa.”

“Wewe na Dennis mko sawa?”

“Mimi na bwana wangu tunaamini katika jambo hili usawa. Hata mimi ninaweza kutoa maoni yangu mbele ya bwana wangu...”

“Mama Resi, jambo la usawa linakuharibu mawazo yako bure. Jambo la maana katika jamii yoyote ni heshima. Bwana na mke, hata kama wanajidai kwamba wao ni sawa, wasipopeana heshima jamii yao haitakuwa thabiti kamwe.”

Katika dondoo hilo tunaona Tumaini akipambanishwa na Mama Resi katika mazungumzo. Ni katika mazungumzo hayo ndipo tunapogundua mitazamo ya wahusika hawa kuhusu usawa kati ya mwanamume na mwanamke. Kupitia mazungumzo hayo msimulizi-mwandishi anawasawiri wahusika hawa kuwa ni watu waliokuwa wakitofautiana kimtzambo na kifikra. Wakati Tumaini anasawiriwa kama mtu aliyekuwa akiamini katika heshima; Mama Resi anasawiriwa kama mtu aliyekuwa akiamini katika haki na usawa wa kijinsia. Usawa huo anaouamini Mama Resi, kwa Tumaini ulikuwa ni usawa uliojikita katika mtazamo wa Kizungu wakati kwa mtazamo wa Kiafrika usawa ni wa kuheshimiana (ukurasa wa 72). Kutokana na mazungumzo hayo, pia inaibuliwa dhamira ya Uafrika dhidi ya Umaghari. Katika dhamira hii tunaelezwa kuwa kwa mtazamo wa Kiafrika heshima ni jambo la msingi wakati kwa mtazamo wa Kimaghari usawa wa kijinsia ndio jambo la msingi bila kujali iwapo usawa huo unazingatia utu.

Pia, mbinu hii imetumika kuwapambanisha Tumaini na Dennis katika mazungumzo yao. Kupitia mazungumzo yao (ukurasa wa 63-64) tunabaini mtazamo wa kila mhusika kuhusu maisha. Katika ukurasa wa 63 Tumaini anasawiriwa kama mtu aliyeamini kuwa, ulimwengu hauwezi kuwa na taabu kama mtu ana pesa, nyumba, na gari. Wakati Tumaini akisawiriwa hivyo, Dennis anasawiriwa kama mtu aliyeamini kuwa furaha ya mwanadamu haiwezi kuletwala na vitu kama nyumba hasa ukizingatia kuwa “nyumba za binadamu zinaonesha upungufu wa uhuru alionao” (ukurasa wa 64). Kutoka na mbinu hii ya mazungumzo tunaweza kubaini ujumbe ambao

msimulizi-mwandishi anataka tuupate. Mathalani, katika ukurasa wa 64 tunaelezwa kupidia Dennis kuwa furaha katika maisha hailetwi na wingi wa vitu ambavyo mtu anavimiliki.

Aidha, Leonila na Anastasia wamepambanishwa ili kubainisha uhusiano wao. Katika riwaya hiyo inaonekana Leonila na Anastasia walikuwa marafiki kabla ya kuhitilafiana kutokana na wote kumuhitaji Tumaini. Kuhitilafiana huko kunasawiriwa kwa kutumia mazungumzo yao katika ukurasa wa 25-26:

“Vipi dada; mbona hivi!”
 “Mimi sikuelewi,” Anastasia alijibu.
 “Mbona umenipindulia serikali yangu!”
 “Nani amekwambia!”
 “Nimesikia kwamba kitanda cha bwana wangu siku hizi kimekuwa chako!”
 “Sikufahamu kama alikuwa amekwisha toa mahari! Tangu lini dada yangu, huyu akawa bwana wako?”
 “Hufahamu kwamba ninamtunzia mtoto wake!”
 “Samahani dada yangu, ye ye mwenyewe aliniambia kwamba amekwisha kupiga chaki.”
 “Umesema nini? Sema tena nisikie!”

Katika dondo hilo Leonila na Anastasia wanachorwa wakiwa wanazungumza. Wahusika hawa wanawiriwa kama watu waliokuwa marafiki lakini baadaye walihitilafiana kwa sababu ya kugombea mwanamume, Tumaini. Kupidia dondo hilo, uhusiano kati ya wahusika hawa unaonekana kubadilika kutoka ule wa kirafiki na kuwa wa kiuadui. Hivyo, zaidi ya kusawiriwa kwa uhusiano baina ya Leonila na Anastasia, pia unasawiriwa mgogoro wa kimapenzi uliopo baina ya wahusika hao.

3.6 Mbinu ya Uwasilishaji Dhahiri

Mbinu hii inahusisha kutaja moja kwa moja na kwa uwazi sifa za mhusika fulani katika matini husika. Hii ina maana kwamba sifa na matendo ya mhusika yanaelezwa waziwazi na msimulizi. Mbinu hii ya kuwaumba wahusika husaidia kumfanya msomaji asipate taabu katika kutambua wasifu wa ndani na wasifu wa nje wa mhusika. Pia, mbinu hii humsaidia msomaji kutambua kiini cha kisa, wazo au dhamira (Msokile, 1992:43).

Katika riwaya hii, mbinu ya uwasilishaji dhahiri imetumiwa na msimulizi-mwandishi katika kuwajenga wahusika wake. Miiongoni mwa wahusika waliojengwa kwa kutumia mbinu hii ni Dennis. Katika riwaya hii tunaelezwa kwa uwazi kuwa, “Dennis alikuwa kifungua mimba” (uk. 5), na “aliishi kwenye nyumba kubwa” (ukurasa wa 60). Maelezo haya kuhusu Dennis yanaonesha wazi kuwa mtu huyo alikuwa ni nani

na aliishi maisha ya namna gani. Kwa mfano, tunaelezwa wazi kuwa Dennis aliishi kwenye nyumba kubwa ya serikali; hali hii inamjenga Dennis kama mtu aliyekuwa na unafuu wa maisha kuliko watu wengine.

Mhusika mwingine aliyejengwa kwa kutumia mbinu hii ni Mulele. Mhusika huyu anaelezwa kama mtu ambaye “alikuwa akijishughulisha na kilimo” na ambaye “alikuwa akiupinga ujamaa” (ukurasa wa 33). Zaidi anajengwa kama “mtu mkarimu” (ukurasa wa 38) na ukarimu wake unaelezwa wazi kuwa alikuwa akitengeneza pombe na kuwakaribisha jirani zake kunya bila malipo. Kutokana na maelezo hayo, tunaweza kumuelezea Mulele kama kiwakilishi cha watu ambao hawakuwa tayari kuupokea ujamaa kwa sababu tayari wao walikuwa wakiishi kijamaa katika vijiji vyao kwani walikuwa wakishirikiana katika masuala mbalimbali. Kutokana na kusawiriwa huko, tunabaini dhamira ya ukarimu, na zaidi tunajuzwa kuwa ujamaa ni jadi ya Waafrika.

Mhusika mwingine aliyesawiriwa kwa kutumia mbinu hii ni John, rafikiye Tumaini. Katika ukurasa wa 47, msimulizi-mwandishi anamsawiri John kwa uwazi kuwa, “aliacha shule alipofukuzwa baada ya kuwagomesha wenzake kula chakula,” na “aliishi kama mhuni.” Kutokana kusawiriwa huko, kadiri simulizi inavyoendelea tunaelezwa John akifanya matendo ambayo hayakubaliki kama vile, kufanya tendo la ndoa na wake wa rafiki zake, ulevi, na kadhalika. Matendo haya hayana budi kufanywa na mhusika huyu kutokana na namna alivyosawiriwa tangu mwanzo. Mbinu hii, zaidi ya kumsawiri John, inaibua dhamira mbalimbali kama vile uhuni, umuhimu wa elimu, na kadhalika.

4.0 Hitimisho

Tunapochunguza kuhusu mbinu zilizotumika kuwajenga wahusika, zaidi ya kusawiri sifa za wahusika na kudokeza dhamira, zimefanikisha kufafanua falsafa iliyofumbatwa katika jina la riwaya: *Dunia Uwanja wa Fujo*. Falsafa hii inayaona maisha kuwa ni fujo tupu (Senkoro, 2011). Fujo hizi zinaonekana kila mahali, vijijini mpaka mijini. Aidha, fujo hizi zinaokana katika maeneo mbalimbali kama vile; katika siasa, lugha, ndoa, na kadhalika. Kwa mfano, katika mbinu ya matendo tumeeleza matendo kadhaa kama ya Tumaini kumtorosha Anastasia; Mama Resi kukataa kushuka kwenye basi na kadhalika. Matendo haya yanasiwiri fujo zinazoendelea ulimwenguni. Kitendo cha Tumaini kumtorosha Anastasia ni fujo kwa jamii kwa sababu misingi ya ndoa inakiukwa. Aidha, kitendo cha Mama Resi kutoshuka kwenye basi ni fujo. Kimsingi matendo hayo yanadokeza falsafa iliyofumbatwa katika jina la kitabu. Kwa hivyo, mbinu zilizobaishwa katika makala haya zina mchango mkubwa katika kuelewa mawazo ya riwaya au falsafa inayohusika.

Marejeleo

- Bal, M. (1997). *Narratology: Introduction to the Theory of Narrative* (2nd edition). Toronto: University of Toronto Press.
- Diegner, L. (2002). “Allegories in Euphrase Kezilahabi’s Early Novels,” katika *Swahili Forum IX*, uk. 43-74.
- Kezilahabi, E. (2007). *Dunia Uwanja wa Fujo*. Nairobi: Vide-Muwa Publishers Limited.
- Madumulla, J. S. (2009). *Riwaya ya Kiswahili*. Dar es Salaam: Mture Educational Publishers.
- Mlacha, S. A. K. (1991). “Point of View as Stylistic Device in Kiswahili Novels,” katika *Kiswahili: Jarida la Taasisi ya Uchunguzi wa Kiswahili*, Juz. 58, kur. 54-61. Dar es Salaam: TUKI.
- Mohamed, S. A. (1995). *Kunga za Nathari ya Kiswahili: Tamthilia, Riwaya na Hadithi Fupi*. Nairobi: East African Educational Publishers.
- Mohochi, E. S. (2000). “Usimulizi wa Riwaya ya Nyongo Mkalia Ini” katika *Nordic Journal of African Studies* 9 (2), uk. 49-59.
- Msokile, M. (1999). *Misingi ya Hadithi Fupi*. Dar es Salaam: Dar es Salaam University Press.
- Mulokozi, M. M. (1983). “*Dunia Uwanja wa Fujo* (Mapitio ya Kitabu),” katika *Kiswahili: Jarida la Taasisi ya Uchunguzi wa Kiswahili*, Juz. 50/1, kur. 1-12. Dar es Salaam: TUKI.
- Njogu, K. & Chimerah, R. (2008). *Ufundishaji wa Fasihi: Nadharia na Mbinu* (Chapa ya Pili). Nairobi: Jomo Kenyatta Foundation.
- Senkoro, F. E. M. K. (1982). *Fasihi*. Dar es Salaam: Press and Publicity Centre.
- Senkoro, F. E. M. K. (2011). *Fasihi*. Dar es Salaam: KAUTTU.
- Shen, F. (2006), “Narrative Strategies in Robert Cormier’s Young Adult Novels.” PhD Dissertation, Ohio State University.
- Wafula, R. (2002). “Language and Politics in East African Swahili Prose: Intertextuality in Kezilahabi’s *Dunia Uwanja wa Fujo* ‘The World a Playground of Chaos,’” katika Obeng, S. G. & Hartford, B. (wah.), *Surviving Through Obliqueness: Language of Politics in Emerging Democracies*, uk. 19-29. New York: Nova Science Publishers Inc.
- Wamitila, K. W. (1997). “*Contemptus Mundi* and *Carpe Diem* Motifs in Kezilahabi’s Works” katika *Kiswahili: Jarida la Taasisi ya Uchunguzi wa Kiswahili*, Juz. 60, kur. 15-24. Dar es Salaam: TUKI.
- Wamitila, K. W. (2008). *Kanzi ya Fasihi: Misingi ya Uchanganuzi wa Fasihi*. Nairobi: Vide-Muwa Publishers Ltd.